# MASWALI NA MAJIBU YA SAILI MBALIMBALI ZILIZOFANYIKA MAENEO YA HALMASHAURI, MANISIPAA PAMOJA NA MAJIJI MBALIMBALI NCHINI TANZANIA KATIKA NAFASI YA KAZI YA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA TATU.

assengaonline.com

**QN1.Kila Afisa mtendaji wa kijiji anatakiwa kutunza daftari lamali zakudumu.Daftari hilo litaonyesha mambo gani? yaeleze kwa upana.**

a) Aina ya mali ya kudumu,hati na mahali ilipo.
b) Jina la mmiliki.
c) Gharama ya mali ya kudumu.
d) Tarehe ya kununulia mali ya kudumu.
e) Ongezeko la thamani ya mali ya kudumu.
f) Mauzo na taarifa nyingine kuhusu mali ya kudumu.
g) Kila aina ya mali iliyoandikwa kwenye ukurasa wa peke yake

**QN2.Mambo gani ya kuzingatia katika tahadhari ya majanga? yaelezee.**

a) Hatua ya kwanza kubuni taratibu,mbinu na mikakati ya kuzuia majangailiyasitokee au kupunguza athari zake pindi yanapotokea.
b) Hatua ya pili kuwezesha jamii kufuata taratibu zote za kutekeleza mbinunamikakati ili kujenga uwezo kwa jamii kudhibiti majanga yasitokee.

**QN3.Eleza njia kuu za kudhibiti mapigano katika jamii?**

a) Kuimarisha utawala bora katika ngazi zote za halimashauri yaani ngazi zamitaa,vijiji na kata.
b) Kuhamasisha uelewa kuhusu misingi ya utawala bora katika ngazi zote.
c) Kujenga umoja wa kuheshimiana na kushirikiana katika makundimbalimbali katika jamii moja.
d) Kujenga umoja wa kuheshimiana na ushirikiano kati ya uongozi na jamii zakijiji au kata au majirani.

**QN4.Ni mambo gani ya kuzingatia ili kikao kiwe halali?**

a) Mahudhurio
b) Mwenyekiti.
c) Katibu.
d) Idadi ya wajumbe.
e) Agenda.
f) Muhtasari.

**QN5.Afisa mtendaji wa kijiji kama mtendaji mkuu wa shughuli zote katika eneo lake na pia kama mlinzi wa amani,unalo jukumu kubwa la kuhakikisha migogoro yote inayojitokeza inashughulikiwa na kupewa ufumbuzi wakudumu.Katika uendeshaji wa**

**shughuli za serikali,uzoefu unaonyesha kuwa katika maeneo mengi hususani kwenye ngazi ya kijiji kuna aina mbalimbali za migogoro.Eleza aina tano za migogoro iliyopo katika ngazi za kijiji utakayotakiwa kushughulika nayo?**

a) Migogoro kati ya koo na koo.
b) Migogoro kati ya kaya na kaya.
c) Migogoro kati ya wananchi na wawekezaji.
d) Migogoro kati ya wakulima na wafugaji.
e) Migogoro kati ya serikali ya kijiji na taasisi za mikopo.

**QN6.Utahakikisha vipi taarifa za makusanyo ya fedha yakiwemoyaushuru,ada na mapato mengine yanakusanywa ndani ya kijiji kwa mujibuwasheria?**

a) Daftari la malipo.
b) Stakabadhi za malipo.
c) Risti mbalimbali.
d) Nyaraka za malipo.

**QN7.Eleza jinsi utakavyosimamia matumizi bora ya rasilimali zaummakatika kijiji chako.**

a) Kupanga.
b) Kuweka wasimamizi.
c) Kuunda vikundi.
d) Njia za udhibiti.
e) Mbinu za mawasiliano.

**QN8.Kitovu cha vita ya umaskini ni kaya.Umaskini na hali duni yamaishavitaweza kumalizika tu iwapo wananchi wenyewe wataamua kuondokana na hali hiyo kwa kutumia nguvu-kazi iliyopo,rasilimali zilizopo kwenye maeneoyao na misaada kutoka serikalini na sehemu nyingine ikiwemo ya wadauwamaendeleo pale hali inaporuhusu.Ili kupunguza na kuondokana na umasikini,Maafisa watendaji wa vijiji au mitaa kwa kushirikiana naviongozina wataalam wengine,wanatakiwa kuchukua hatua mbalimbali,elezahatua tano(5)utakazochukua kukabiliana na hali hiyo?**

a) Kuelewa hali ya umaskini katika maeneo yao.
b) Kuainisha sababu za umaskini kwa kushirikiana na wananchi.
c) Kuelekeza kila mwananchi aelewe tatizo la umaskini na ajenge azmayakufanya kazi kwa bidii ili kuondokana na umaskini.
d) Kuwaeleza wananchi kutumia fursa zilizopo ili kuondokana na hali hiyo.
e) Kuunda vikundi vitakavyosaidia kuepukana na hali ya umaskini.

**QN9.Moja kati ya majukumu na kazi za kamati za halmashauri yakijiji nikuhakikisha kuwa kanuni za kilimo bora na malengo ya kilimo,ufugaji borana uvuvi bora zinafuatwa na kutekelezwa.Taja namna utakavyotekelez**a?

a) Kutayarisha mashamba mapema,
b) Kusafisha mashamba baada ya mavuno.
c) Kupanda mapema kwa kufuata mazingira ya hali ya hewa.
d) Kuhifadhi mazao gharani.

e) Kuchagua mbegu bora na kuweka mbolea mashambani.

assengaonline.com

**QN10.(a) Taja mambo makubwa ya kimuungano ambayo Tanzaniabaranavisiwani wanashirikiana.**

i. Katiba ya jamhuri na serikali ya Jamhuri ya Muungano.
ii. Mambo ya Nchi za Nje.
iii. Ulinzi na Usalama.
iv. Polisi.
v. Mamlaka juu ya mambo yanayohusika na hali ya hatari.
vi. Uraia.
vii. Uhamiaji.
viii. Mikopo na biashara ya Nchi za Nje.
ix. Utumishi katika serikali ya Jamuhuri ya Muungano.
x. Kodi ya mapato inayolipwa na watu binafsi na mashirika,ushuru waforodhana ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania.
xi. Bandari,mambo yanayohusika na usafiri wa anga,posta na simu
xii. Mambo yote yanayohusika na sarafu na fedha kwa ajili ya malipoyotehalali(pamoja na noti);mabenki(pamoja mabenki ya kuweka akiba) nashughuli zote za mabenki;fedha za kigeni.
xiii. Leseni ya viwanda na takwimu.
xiv. Elimu ya juu.
xv. Maliasili ya mafuta,pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa namafutaya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa,na gesi asilia. xvi. Baraza la taifa la mitihani la Tanzania na mambo yote yanayohusikanakaziza Baraza hilo.
xvii. Usafiri na usafirishaji wa anga. xviii. Utafiti.
xix. Utafiti wa hali ya hewa.
xx. Takwimu.
xxi. Mahakama ya Rufani ya Jamuhuri ya Muungano.
xxii. Uandikishaji wa vyama vya siasa na mambo mengine yanayohusiananavyo.

**(b) Taja viashiria vitano vya umaskini hapa Tanzania.**

i. Kutokujua kusoma na kuandika.
ii. Kutokuwa na uhakika wa kupata chakula,mavazi na malazi.
iii. Uhaba wa maji safi na salama.
iv. Huduma duni za afya.
v. Vifo vingi vya wananchi.
vi. Muda mfupi wa maisha.
vii. Utapiamlo kwa watoto na watu wazima.
viii. Uchakavu wa mazingira.
ix. Ukosefu wa ajira na kipato duni.
x. Kutokufahamu masuala muhimu ya jamii.

**QN11.Ukiwa kama mtendaji wa kijiji utakutana namajalada, nyarakambalimbali za serikali na vitu vingine vingi katika kazi zako za kilasiku.Jenimambo gani muhimu ya kuzingatia unapokutana na nyaraka hizo?**

a) Kuhakiki hizo nyaraka.
b) Kuzichambua hizo nyaraka.
c) Kuzipanga na kuzitofautisha
d) Kuzihifadhi/kuzitunza kwa kila nyaraka katika majalada(file) lakekatikamasijara.

**QN12.Taja majukumu ya mkutano mkuu wa kijiji.**

a) Kupokea na kujadili taarifa za utekelezajiwa shughuli mbalimbali.
b) Kupokea na kujadili mapato na matumizi ya fedha.
c) Kupokea na kujadili taarifa za makusanyo ya fedha yakiwamo ya ushuru,adana mapato mengine yanayopaswa kukusanywa ndani ya kijiji kwamujibuwa sheria.
d) Kupokea na kujadili taarifa za watu walioomba kupewa ardhi.
e) Kupokea na kujadili mapendekezo yaliyotolewa na halmashauri ya kijiji aukitongoji.
f) Kufanya maamuzi yanayozingatia demokrasia.
g) Kuchagua mwenyekiti na wajumbe wa halmashauri ya kijiji.
h) Kujadili na kupitisha bajeti na mipango ya maendeleo.
i) Kuidhinisha utungwaji wa sheria ndogo kabla ya kupelekwa kwenyehalmashauri wilaya kwa ajili ya kupitishwa kwa manufaa ya kijij.

**QN13.Taja misingi ya utwala bora.**

a) Utawala wa sheria.
b) Demokrasia.
c) Ushirikishwaji.
d) Uwazi.
e) Uwajikibikaji.
f) Ufanisi.

**QN14.Taja vyanzo vitano vya mapato halmashauri za wilaya?**

a) Mapato ya ndani.
b) Wahsani/wafadhili.
c) Mikopo kutoka taasisi mbalimbali za fedha kama vile banki n.k
d) Michango ya jamii.
e) Ruzuku kutoka serikali kuu.

**QN15. Taja alama muhimu za taifa?**

a) Mwenge wa uhuru.
b) Wimbo wa taifa.
c) Bendera ya taifa.
d) Fedha ya taifa.
e) Nembo ya taifa.

**QN16. Taja maadili matano(5) ya utumishi wa umma?**

a) Kufanya kazi kwa bidii.
b) Kutoa huduma bila upendeleo.
c) Utii kwa serikali.
d) Kutokupokea rushwa.
e) Kutunza siri za serikali.
f) Kutoa huduma bora.
g) Kufanya kazi kwa uadilifu.
h) Uwajibikaji kwa umma.
i) Kuheshimu sheria.
j) Matumizi sahihi ya taarifa

**QN17. Taja rangi za bendera ya Tanzania na maana zake.**

a) Nyeusi-Inawakilisha watu wa Africa.
b) Njano-Inawakilisha madini.
c) Kijani-Inawakilisha mimea.
d) Bluu-Inawakilisha mito,maziwa na bahari.

**QN18. Taja majukumu ya Afisa mtendaji wa kijiji.**

a) Atakuwa mtendaji na mshauri mkuu wa serikali ya kijiji na kamati zakekatika mipango ya maendeleo ya jamii na utekelezaji wa mipangoyamaendeleo.
b) Atakuwa Afisa mhasibu wa serikali ya kijiji na atasimamia mapatonamatumizi yz serikali.
c) Atakuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
d) Ataratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleoya kijiji.
e) Atakuwa katibu wa kamati ya halmashauri ya kijiji.
f) Atatafsiri sera,ataratibu na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogodondogo.
g) Atawajibika kwa mtendaji wa kata.
h) Atakuwa kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika kijiji.
i) Atasimamia matumizi bora ya nguvu kazi.
j) Atahamasisha wananchi katika kampeni za kuondoa njaa,umaskini nakuongeza uzalishaji mali.
k) Atasimamia ukusanyaji wa kumbukumbu za walipa kodi,wataalamumbalimbali na NGOs waliopo katika kijiji.

**QN19.In state set up! What does separation of power mean?**

Separation of power-Refers to the states being separated and vested inthethreeorgans/branches of the states. These branches are The Legislature, The judiciaryand The executive Functions of each organ

a) The legislature
i. To make and amend laws.
ii. To discuss and pass the budget.

iii. To question ministers during parliamentary season.
b)The judiciary
i. To interpret laws.
ii. To provide rights for injury or harm person.
c) The executive To enforce laws and to ensure everyone obey the laws.

**QN20. (a)Village governments have been given a mandate to make by-laws;Which institution has delegated this function?**
-The institution delegating this function is the legislature
(b) What is good governance?
-Is a way of measuring how public institutions conduct public affairs and manage public resources in a preferred way.
(c) Mention any five pillars of good governance?
i. Rule of law.
ii. Democracy.
iii. Participatory.
iv. Transparency.
v. Accountable.
vi. Responsiveness.
vii. Consensus oriented.
viii. Effective and efficiency.

QN21. LGAs have various sources of revenue. Can you mention at least 3 sources of revenue for the following categories of LGAs. (a) District councils? (b)Urban councils? (c) Village government?
**There are five main sources of revenue in District & urban councils these include**
i. Own source.
ii. Donors.
iii. Borrowing
iv. Community contributions.
v. Intergovernmental transfer.

**-Sources of revenue in village government**
i. Fine and penalties
ii. Percent of the unit or field sales/mauziano ya kiwanja ushamba kuna asilimia(10%) kijiji huwa kinachukua.
iii. Any other sources of revenue passed by village assembly.

**QN22. Mention any five roles of local government to community development?**
a) To formulate, coordinate and supervise the implementation of all plans for the economic, commercial, industrial and social development in its area of jurisdiction.
b) To ensure the collection and proper utilizations of the revenues.
c) To regulate and monitor the collection and utilization of revenue of village councils and township authorities.

d) Take all necessary measures for the prevention of soil erosion and the protection of crops.
e) To prepare, undertake, regulate and control schemes for improved housing layout and settlement.
f) To provide services for the improvement of livestock.

**QN23.Nini maana ya Afisa mtendaji?**
-Ni mtu mwenye utaalamu katika eneo au taasisi, ambapo kazi yake ni kufuatilianamna taasisi zinavyofanya/kutenda kazi mara nyingi mtendaji ni mtuwakuajiriwa tofauti na viongozi wanaochaguliwa na wananchi.

assengaonline.com

**QN24. Define the following terms.**
i. Local government Authority. Is a type/kind of government vested powers to perform functions within the specified areas.
Examples of local government authorities a) Rural authorities District councils, Township Authorities and village councils b) Urban Authorities ; City council, Municipal and Town council
**ii. By-laws**. Is a rule or law established by an organization to regulate itself as allowed or provided for by some higher authority .OR By-law can be defined as a law of local or limited application passed under authority or higher law stating things they may regulate.
**iii. Rule of law**. Is a situation in which the laws of the country are obeyed by everyone.

QN25**.(a) How many types of councilors do we have in council.**
-According to the book of " MJUE DIWANI" there are four(4) typesofcouncilors i)Elected councilors. ii) Appointed councilors. iii)Such a number of women members who are qualified to be elected to the council. iv) Member of parliament representing constituencies .
**(b) How councilors elected?**
-According to the book of "mjue diwani" how councilors elected? Elected during general election which held for every five years. Elected during by election when a member dies, resigns ,his election voided by court, member ceased to be a member of the political party that sponsored him. Such a number of women members who are qualified to be elected to the council.

QN26. **(a) Bunge ni nini?**
-Ni chombo cha kutunga sheria ambacho kimepewamamlaka kwa mjibu wa katiba ya Jamuhuri ya muungano wa Tanzania yamwaka1977 ibara ya 4,61,64 .
(**b) Kuna aina mbili za bunge zitaje?**
i)Bunge la chumba kimoja ambako wawakilishi wote wa wananchi hukaapamoja na kufanya maazimio pamoja.
ii)Bunge la vyumba viwili ambako kitengo kikubwa kina kazi ya kutungasheria na wabunge huchaguliwa moja kwa moja na wananchi katikamajimbo ya uchaguzi.

**QN27. Ni faida zipi zinazoweza kudumisha utamaduni bora waTaifaletu?Taja angalau tano.**

a) Kutambua na kulinda rasilimali,mazingira na urithi wa utamaduni.

b) Kuhakikisha na kuhimiza usawa katika matumizi bora na mgawanyowahaki na rasilimali.

c) Utamaduni husaidia kuenzi na kutunza tabia njema na kukemea vitendoviovu kama vile matumizi ya madawa ya kulevya,ubakaji,unyanyasaji n.k

d) Utamaduni husaidia kutambua na kuhimiza kazi halali kuwa ni msingi wamaisha na maendeleo ya binadamu.

e) Kuhimiza utunzaji wa rasilimali za Taifa.

f) Kupiga vita udhalilishaji wa kijinsia.

g) Kuhimiza tabia ya kuheshimu utu,watu na sheria kwa manufaayamaendeleo.

h) Kujenga tabia ya usafi ,uhifadhi na matumizi bora ya rasilimali na mazingira.

i) Utamaduni husaidia kuhimiza na kujenga Taifa lenye nidhamu.

j) Kujenga taifa na kutambua,kuenzi na kuheshimu vitambulisho vya Taifa.

**QN28.Tanzania iliamua rasmi kuingia rasmi kwenye mfumo wa vyama vingi mnamo mwaka 1992.Lengo la mfumo huu ni kuleta ushindani naufanisikatika kuwahudumia wananchi na kupanua wigowauwazi,ukweli,uwajibikaji,na utawala bora kwa ujumla nasivinginevyo.Miongoni mwa taratibu zinazopaswa kufuatwa katikakujengademokrasia ya kweli ni pamoja na watu kujijengea utamaduni .Elezatamaduni hizo.**

a) Uvumilivu na staha kwa mitazamo na maoni tofauti ya kisiasa.

b) Kufuata na kuheshimu mawazo ya walio wengi na pia kusikiliza na kukubalimawazo ya wachache iwapo yana manufaa na umuhimu mkubwakwakitongiji au mtaa,kijiji,kata,wilaya,mkoa au Taifa kwa ujumla.

c) Kutumia nguvu ya hoja na siyo hoja za nguvu.

d) Kupingana bila kupigana.

e) Kujikosoa na kukosoana bila kuleana.

assengaonline.com

**QN29.Taja majukumu ya kamati ya fedha,uchumi na mipango.**

a) Kubuni miradi mbalimbali ya maendeleo kijijini.

b) Kuweka hesabu sahihi za shughuli zote kijijini.

c) Kupendekeza matumizi bora ya ardhi ya kijiji kwa ajili ya shughulimbalimbali za kilimo,ufugaji na ujenzi.

d) Kusimamia ukusanyaji wa kodi na ushuru uliowekwa na Halmashauri yawilaya na Serikali ya kijiji.

e) Kutafuta njia mbalimbali za kuongeza mapato kijijijini.

f) Kuhakikisha kanuni bora za kilimo na malengo ya kilimo,ufugaji nauvuvibora zinafuatwa na kuendelezwa.

**QN30.Taja mbinu za kutatua migogoro katika jamii.**

a) Kutawala maamuzi.

b) Mbinu shirikishi.
c) Kuepuka suluhu ya mgogoro.
d) Kuepusha shari.
e) Kukubaliana.

**QN31.Maafisa watendaji wa kijij wamepewa uwezo wa kukamata aukuagizakukamata kutokana na sheria zipi? Zitaje.**
a) Sheria ya serikali za mitaa(mamlaka za wilaya) Namba 7 ya mwaka 1982.
b) Sheria ya serikali za mitaa(mamlaka za miji) Namba 8 ya mwaka 1982.
c) Sheria ya mwenendo wa kesi za jinai Namba 9 ya mwaka 1985.
d) Sheria ya mahakama za mahakimu Namba 2 ya mwaka 1984.

**QN32.Taja sababu ambazo zinasababisha serikali kusisitiza maendeleovijijini?**
a) Kijijini ndipo mahali shughuli za kilimo zinapofanyika ambapokilimoniutii wa mgongo wa Taifa.
b) Miundo mingi vijijini haipatikani mfano barabara,huduma za afya n.k
c) Uelewa mdogo miongoni mwa wananchi hasa wanaoishi vijijini.
d) Kipato duni miongoni mwa wananchi wanaoishi vijijini na wenginekushindwa kumudu mahitaji muhimu.

assengaonline.com

**QN33. Taja msingi ya kidemokrasia. a) Ushirikishwaji wa wananchi.**
b) Kujikomboa.
c) Madaraka kwa umma.
d) Uchaguzi huru na haki.
e) Uhuru wa binafsi.
f) Haki za binadamu na wajibu (sura ya kwanza sehemu ya tatu (12-25) yakatiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977)
g) Mgawanyo wa madaraka na vyombo vikuu vya uongozi wan chi ambavyonibunge,serikali na mahakama.

**QN34. Taja walinzi wa amani.**
a) Wakurugenzi wa Halmashauri za wilaya,miji,manisipaa au jiji.
b) Afisa Tarafa.
c) M aafisa watendaji wa vijiji au mitaa.

**QN35.Eleza nafasi ya Afisa mtendaji wa mtaa katika utekelezaji waulinzishirikishi?**
a) Kushawishi wananchi katika kijiji/mtaa kuanzisha mtandao waulinzishirikishi kwa kushirikiana na kamati ya ulinzi na usalama ya kijiji namtaa.
b) Kuratibu shughulu zote za mtandao wa ulinzi shirikishi.

c) Kuitisha mikutano ya ujirani mwema,kutangaza mpango wa ulinzi shirikishikwa nguvu zote ili kila mwananchi aone umuhimu wa kushiriki katikanakufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kujua maeneo yenye udhaifuambayoyanaweza kutumiwa na wahalifu.

d) Kushirikiana na jeshi la polisi na vyombo vingine vya dola sambambanaaskari wa Halmashauri katika utekelezaji wa mikakati ya kuzuia uhalifunavurugu kwa kuihusisha jamii. ndugu zangu ikumbukwe kwamba haya ni mawazo ya wadau pamojanagroupletu la questions for interviwes kilichofanyika ni kuunganisha mawazohayo, maswali mengine bado hayajapatiwa majibu yakiwa tayari tutatuma.

**JIUNGE HAPA**